


**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**



TANGAZO LA ZABUNI

1. LGA/009/HQ/2018/2019/N/01/4: KUTOA HUDUMA YA USAFI WA NDANI KATIKA HOSPITALI YA WILAYA

MAOMBI YA ZABUNI

KIPINDI CHA 2018/2019

Tarehe: 07/01/2019

1. Halmashauri ya wilaya kisarawe imetenga fedha kwa ajili ya kupata huduma ya Usafi wa ndani katika majengo ya Hospitali ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
2. Halmashauri ya wilaya Kisarawe inapenda kuwaalika watu binafsi Makampuni Mashirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia ya uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao ya zabuni hii.
3. Waombaji wanakaribishwa kutembelea maeneo ya kazi na kupata ufanuzi wa yaliyomo katika nyaraka za zabuni. Kazi zote zipo katika eneo la Hospitali ya Wilaya Kisarawe
4. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo;
 - i). Nyaraka za zabuni zitapatikana kwa malipo ya Tsh 100,000/=(mia moja elfu) ambayo haitarejeshwa kwa kila fungate. Mwombaji atatembelea eneo la kazi kabla kuchukua nyaraka ya zabuni ambayo itatolewa eneo la kazi
 - ii). Ombi la zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (physical address)
 - iii). Zingatia kuwa fom ya maombi ya zabuni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria ‘ Power of Attorney’
 - iv). Leseni halali ya biashara.
 - v). Uthibitisho wa mlipa kodi Tin/VAT
5. Mwombaji aonyeshe vifaa alivyonavyo maelezo na wataalamu alionao, sifa zao na uzoefu.
6. Mwombaji awasilishe nakala halisi na nakala mbili zilizozalishwa endapo maelezo ya nakala zilizozalishwa na nakala halisi yatatofautiana nakala halisi ndio itatumika kwenye tathimini.
7. Zabuni ijazwe vizuri,iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote na juu ya bahasha iandikwe namba ya zabuni, jina la kazi inayoombwa , Bahasha iandikwe kuwa na nakala halisi au nakala iliyozalishwa, kisha iandikwe anuani tajwa
8. Uongozi haulazimiki kuchagua zabuni yoyote
9. Zabuni zote zifungwe kwa lakiri na bahasha juu iandikwe kwa herufi kubwa jina la zabuni iliyoombwa na namba ya zabuni. Maombi yatumwe kwa:

KATIBU WA BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 28001
KISARawe.

- 10 Mwisho wa kupokea zabuni hizo ni tarehe 14/01/2019 saa nne (4:00) asubuhi. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo saa 4:30 asubuhi. Waombaji au wawakilishi wa makampuni wanaombwa kuhudhuria siku ya ufunguzi wa zabuni
10. Maelekezo na masharti mengine ya zabuni yapo ndani ya kitabu cha zabuni husika. Kitabu cha zabuni kinapatikana katika ofisi ya katibu wa Bodi ya zabuni siku zote za kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi mpaka 9.30 alasiri
11. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi ambaou utafanyika mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo.
12. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao(e-mail) hazitapokelewa
13. Anuani ya kutuma zabuni hizo ni

KATIBU WA BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 28001
KISARawe.

